


## AFYA
SHA yafikia usajili wa milioni 24.8 huku TAIFA Care ikizidi kushika kasi UK 5




## UTHIBITISHO
KEBS kutambuliwa kimataifa kwa uthibitisho wa bidhaa na maabara UK 18

www.gaa.go.ke
Julai 29, 2025
MyGov.
TATHMINI YAKO YA WIKI
TOLEO La. 5/2025-2026

# KRA yavuka shabaha ya mapato kwa Sh16 bilioni




Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Ushuru nchini (KRA), Bw Humphrey Wattanga

**Kamishna Mkuu wa KRA Bw. Humphrey Wattanga anasema ukuaji mkubwa ulirekodiwa katika sekta muhimu kama vile kilimo, misitu na uvuvi; shughuli za kifedha na bima; usafirishaji na uhifadhi; na mali isiyohamishika**

**NA MICHAEL OMONDI (KNA)**

Mamlaka ya Ukusanyaji Ushuru nchini Kenya (KRA) imevuka lengo lake la ukusanyaji mapato kwa mwaka wa kifedha 2024/2025, baada ya kukusanya jumla ya Shilingi trilioni 2.571 dhidi ya lengo la Shilingi trilioni 2.555. Hii ni ongezeko la asilimia 6.8 katika ukusanyaji wa mapato na kiwango cha utekelezaji wa asilimia 100.6, ikilinganishwa na Shilingi trilioni 2.407 zilizokusanywa katika mwaka wa kifedha uliopita.

Kulingana na Kamishna Mkuu wa KRA, Bw. Humphrey Wattanga, ufanisi huu wa mapato unaonyesha hali ya kiuchumi nchini, hasa kwa kuzingatia ukuaji wa Pato la Taifa (GDP) kwa asilimia 4.7 kama ilivyoripotiwa kwenye Ripoti ya Uchumi. Ukuaji mkubwa ulirekodiwa katika sekta kuu kama kilimo, misitu na uvuvi; shughuli za kifedha na bima; usafirishaji na uhifadhi; na sekta ya mali isiyohamishika. Aidha, mfumuko wa bei kwa ujumla ulipungua hadi wastani wa asilimia 3.6 katika

ENDELEA UK 2

## Takwimu za Wiki

**1.3b**
Kiasi cha pesa kaunti ya Garissa itapokea kwa miradi ya nyumba pekee, kulingana na Mratibu wa Kaskazini Mashariki wa Nyumba na Masoko ya bei nafuu.

**1.4b**
Gharama ya mradi wa usambazaji wa umeme vijijini Wizara ya Kawi imezindua Kaunti ya Kericho

**1000**
Idadi ya ambao Mamlaka ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukame (NDMA) inasambaza katika Kaunti Ndogo ya Baringo Kaskazini.

**6b**
Kiasi cha ada za makazi ambazo hazijalipwa Wizara ya Ardhi inapanga kufuta ili kusaidia waliogawiwa ardhi kukusanya hati miliki ambazo hazijadaiwa nchi nzima.

**1.5b**
Kiasi cha fedha ambacho Idara ya Serikali ya Makazi na Maendeleo ya Miji imeelekeza katika kuboresha makazi yasiyo rasmi.


GAA
Find us also on;
Government Advertising Agency
@MyGovKe
@GAA_Kenya
https://gaa.go.ke
Contacts: mygovads@gaa.go.ke | editorial@gaa.go.ke | director@gaa.go.ke | (+254) 020 4920000/1

ENDELEA KUTOKA UK 1

mwaka wa 2024/25, ikilinganishwa na asilimia 6.3 katika mwaka wa 2023/24. Kiwango cha ubadilishaji wa Shilingi ya Kenya dhidi ya Dola ya Marekani kiliongezeka, kwa wastani wa Sh129.35 kwa Dola moja, ikilinganishwa na Sh144.1 mwaka uliopita. Bei ya mafuta ya kimataifa kwa pipa ilishuka kwa asilimia 12.5, hali iliyochangia kupungua kwa bei ya mafuta katika vituo vya mafuta nchini: petroli kwa asilimia 11.8 na dizeli kwa asilimia 12.2. Hata hivyo, Bw. Wattanga alibainisha kuwa baadhi ya changamoto ziliathiri vibaya ukusanyaji wa mapato. Nusu ya kwanza ya mwaka wa kifedha 2024/25 ilikumbwa na changamoto mbalimbali za kiuchumi, ikiwemo kuahirishwa kwa Mswada wa Fedha wa 2024, viwango vya juu vya riba katika benki, vita vya ushuru vya kimataifa, na migogoro ya kimataifa inayoendelea. Hasa, thamani ya jumla ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje iliongezeka kwa asilimia ndogo ya 0.04 pekee, kutokana na kupungua kwa thamani ya uagizaji wa mafuta na vilainishi (-16.4%) na chakula na vinywaji (-14.6%). Wakati huo huo, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi ilipungua kwa asilimia 2.0, hasa kutokana na kupungua kwa mauzo ya mazao ya bustani (-2.5%) na chai (-15.4%).

# KRA yazidisha lengo lake la mapato kwa Sh16b



Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Ushuru nchini (KRA), Bw Humphrey Wattanga (Kulia) akizungumza katika hafla ya awali.

Kamishna Mkuu aliongeza kuwa upatikanaji wa mikopo kwa sekta binafsi uliendelea kuwa mgumu kutokana na viwango vya juu vya riba kutoka kwa benki za biashara ikilinganishwa na mwaka uliopita. Hata hivyo, inatarajiwa kuwa viwango hivyo vitashuka kufuatia uamuzi wa Benki Kuu ya Kenya (CBK) kupunguza kiwango cha riba kuu hadi asilimia 9.75 mwezi Juni 2025. "Kwa hadi mwisho wa Desemba 2024, mikopo iliyotolewa na benki za biashara kwa serikali ya kitaifa ilikua kwa asilimia 13.9, huku mikopo kwa sekta binafsi ikishuka kwa asilimia 1.1," aliripoti, akiongeza kuwa hali hii inakwamisha matarajio ya uwekezaji na upanuzi wa sekta kuu za uchumi. Licha ya changamoto hizo, Bw. Wattanga alisema kuwa mikakati madhubuti ya KRA ilisababisha mafanikio makubwa katika nusu ya pili ya mwaka wa kifedha, ambapo ukusanyaji wa mapato uliongezeka kwa asilimia 9.1, ikilinganishwa na asilimia 4.5 katika nusu ya kwanza.

# Matumizi ya nishati yafikia rekodi ya juu

NA IMMACULATE CHEBET, MYGOV

Kenya imefikia rekodi mpya ya mahitaji ya umeme, ikigonga megawati (MW) 2,362.28 — hatua muhimu katika matumizi ya nishati kitaifa, yakichochewa na upanuzi wa viwanda, ongezeko la miji, na matumizi ya nyumbani yanayozidi kuongezeka. Afisa Mtendaji Mkuu wa Kampuni ya Kuzalisha Umeme Kenya (KenGen), Mhandisi Peter Njenga, alibainisha kuwa vyanzo vya nishati ya jotoardhi na maji vya KenGen vilichangia sehemu kubwa ya umeme kwenye gridi ya taifa. Kulingana na Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Petroli (EPRA), mitambo ya jotoardhi ya KenGen ilizalisha megawati-saa (MWh) 13,678.35, ambayo ni asilimia 31.85 ya uzalishaji wote, huku mitambo ya umeme wa maji ikizalisha MWh 10,915.93, sawa na asilimia 25.42 ya uzalishaji wa kitaifa. Kwa pamoja, vyanzo hivi viwili vilichangia asilimia 57.27 ya uzalishaji wa kila siku wa umeme nchini Kenya. Mkurugenzi huyo alisema kuwa mchango huo umechangia kwa kiasi kikubwa katika kudumisha uthabiti wa usambazaji wa umeme na kuzuia kukatika kwa umeme. "Wakati mahitaji ya jumla ya nishati yalifikia MWh 42,943.11 — yakiwemo vyanzo vya mafuta, upepo na miunganisho ya kielektroniki kutoka Uganda na Ethiopia — tunafurahia kutambua kwa ni usambazaji wa KenGen unaotegemewa kutoka kwa rasilimali asilia za nchini uliohakikisha uthabiti wa gridi," alisema Bw. Njenga. Aliongeza kuwa mahitaji hayo yalitimizwa bila kuwepo kwa taarifa yoyote ya mgawo wa umeme, jambo linaloonyesha mwitikio madhubuti kutoka kwa waendeshaji wa mfumo. Mhandisi Njenga alieleza zaidi kuwa vituo vya umeme wa maji kama Kiambere vilizidi matarajio, kwa kuzalisha MWh 2,908 — asilimia 23.31 zaidi ya makadirio ya usambazaji.



Afisa Mkuu Mtendaji wa KenGen. Peter Njenga.

REPUBLIC OF KENYA

ICT Authority

## THE INFORMATION AND COMMUNICATIONS TECHNOLOGY AUTHORITY

## KENYA DIGITAL ECONOMY ACCELERATION PROJECT ICTA-PROGRAM IMPLEMENTATION UNIT

## ADDENDUM NO. 1

| | |
|---|---|
| **Name of Assignment:** | **Supply, Delivery and Installation of WiFi routers and related goods for 55 universities and TVETs in Kenya:**<br>**Lot 1: 13 No. Institutions;**<br>**Lot 2: 15 No Institutions;**<br>**Lot 3: 18 No. Institutions;**<br>**Lot 4: 9 No. Institutions;** |
| **RFB Reference No.:** | **KE-ICTA-486639-GO-RFB** |
| **Loan No./Credit No./ Grant No.:** | **IDA 7289-KE and 7290-KE** |
| **Country:** | **Kenya** |
| **Date:** | **21st July 2025** |

To All Interested Bidders

### RE: AMENDMENT OF RFB DOCUMENT THROUGH ADDENDUM NO. 1

In accordance with the Instructions to Bidders ITB 8 [Amendment of Bidding Document], the Client has amended Section II - Bid Data Sheet (BDS) of the issued RFB Document:

| S/ No | Section | Original Bid Submission Deadline | New/ Extended Bid Submission Deadline |
|---|---|---|---|
| 1 | Section II – Bid Data Sheet (BDS) | 31st July 2025 at 1000 Hrs EAT | 14th August 2025 at 1000 Hrs EAT |

This addendum No. 1 forms part of the issued RFB document. All other terms and conditions of the issued RFB document remain unchanged.

**Zilpher Owiti, OGW**
**Ag. Chief Executive Officer**
**ICT Authority**

OFFICE OF THE REGISTRAR OF POLITICAL PARTIES
ORPP

## NOTICE FOR PROVISIONAL REGISTRATION

The Office of the Registrar of Political Parties (ORPP) is established by the Political Parties Act, CAP 7D (PPA) as a State Office within the meaning of Article 260 of the Constitution of Kenya, 2010. The mandate of the ORPP is to register and regulate political parties as well as administer the Political Parties Fund.

In line with Section 5 (2) (a) of the PPA, the Registrar of Political Parties is in the process of provisionally registering the following proposed political parties: -

| S / No | Names | Party Colours | Party Symbol | Slogans | Founder Members |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Restoration Alliance Party (RAP) | Gold, Blue, Red, and white | *Spectacle* | Mambo sawa sawa | 1. Dancun Oduor Otieno<br>2. Adam Paul Maina Mwafrica<br>3. Miriti Valentine Hope Wanjira<br>4. John Karamunya Limakamar<br>5. Philomena Bochaberi Koech<br>6. Esther Kamene Mutio<br>7. Masawa Jenipher Achieng<br>8. Alice Gesare Ratemo |
| 2. | Citizen Alliance for Democratic Affairs (CADA) | Green Blue and White | *Peacock* | Siasa za Maendeleo | 1. Dr George Mugai Kiongera<br>2. Ann Njeri<br>3. Innocent Opondo Omondi<br>4. Boniface Kinoti Mutwiri<br>5. Justus Kabosi Wambua<br>6. Getrude Gatwiri Mwongera |

Particulars of the above-listed proposed political parties have been provided on the ORPP website - **www.orpp.or.ke.**

Any objections may be presented in writing or in person within **seven (7) days** to:

**Office of the Registrar of Political Parties (ORPP)**
**Lion Place, 4th floor, off-Waiyaki way, Karuna Close**
**P O Box 1131-00606**
**NAIROBI**
**Email: info@orpp.or.ke**

**Sophia Sitati**
**Ag. Registrar of Political Parties**

ORPPKenya www.orpp.or.ke



DhowCSD
Central Bank of Kenya

Central Bank of Kenya

# 3 Simple Steps to a Tax-Free Income

## Step 1
### Open a DhowCSD Account
- Go to dhowcsd.centralbank.go.ke, or download the DhowCSD App from the App Store or Play Store
- Provide all the necessary requirements and submit your application
- Your account will be active within 48 hours

## Step 2
### Invest in the Infrastructure Bond
- Review the Prospectus for the two Infrastructure Bonds on Offer
- Choose a Bond to Invest in and make your bid through DhowCSD
- Submit your bid before 10:00 a.m. on Wednesday, August 13, 2025
- Make payment by 2 p.m. on Monday, August 18, 2025

## Step 3
### Enjoy Tax-Free Income
- Infrastructure Bonds provide a tax-free income
- Interest is paid every six months
- Principal will be repaid on the dates outlined in the prospectus

Download the CBK DhowCSD Mobile App
GET IT ON Google Play
Download on the App Store

Follow Central Bank of Kenya on WhatsApp Channels
DhowCSD@centralbank.go.ke

Scan me!

**Central Bank of Kenya**
Haile Selassie Avenue
P.O Box 60000 - 00200
Nairobi, Kenya

Tel: +254 709 081222
Toll-free (USA): +1 (833) 201 0220
Toll-free (Kenya): 0800 720222

comms@centralbank.go.ke
DhowCSD@centralbank.go.ke

# Mradi wa NYOTA kufungua nafasi nyingi za kazi kwa vijana

**NA AMINA BAKARI NA ESTHER MULONGO (KNA)**



**Waziri wa Masuala ya Vijana, Uchumi Ubunifu na Michezo Salim Mvurya, akizungumza wakati wa uzinduzi wa Mpango wa Kitaifa wa Fursa za Vijana Kuelekea Maendeleo (NYOTA) katika Hoteli ya Nairobi.**

Kenya, kwa ushirikiano na Benki ya Dunia, imezindua rasmi Mpango wa Kitaifa wa Fursa kwa Vijana uitwao NYOTA (National Youth Opportunities Towards Advancement). Mpango huu ni hatua ya mageuzi yenye lengo la kuwawezesha vijana zaidi ya 200,000 kote nchini kwa kuwapa fursa za ajira, ujasiriamali, teknolojia ya kidijitali, na nafasi katika sekta ya ubunifu.

Hafla ya uzinduzi iliyofanyika jijini Nairobi iliongozwa na Waziri wa Masuala ya Vijana, Uchumi wa Ubunifu na Michezo, Salim Mvurya, pamoja na Katibu wa Masuala ya Vijana na Uchumi wa Ubunifu, Fikirini Jacobs.

Hafla hiyo iliwakutanisha viongozi wa vijana kutoka kaunti zote 47, washirika wa utekelezaji wa mradi, na wadau kutoka serikalini na sekta binafsi.

Akizungumza wakati wa hafla hiyo, Mvurya alieleza kuwa mpango huo ni hatua muhimu ya kimkakati katika juhudi za serikali za kutumia kikamilifu uwezo wa vijana wa Kenya.

"NYOTA si mradi tu; ni jukwaa la kitaifa la mabadiliko kwa vijana—ni mpango unaolenga kuwapa vijana fursa sawa za kufanikisha ndoto zao," alisema.

Mvurya aliongeza kuwa mchakato wa maombi ni wa kidijitali kikamilifu, unapatikana kupitia simu za mkononi, na umetengenezwa mahususi kuondoa urasimu.

"Huhitaji tena kumfahamu mtu serikalini ili upate fursa za uwezeshaji kwa vijana. Iwapo unataka msaada wa kibiashara au utambuzi wa maarifa uliyonayo, unahitaji tu simu, intaneti, na kitambulisho chako," alisema.

Alibainisha kuwa NYOTA tayari imeanza kupata mafanikio huku idadi ya waombaji ikizidi matarajio, na sasa inajiandaa kwa awamu za utekelezaji.

Mvurya alisifu uwazi katika shindano la kuchora nembo ya mradi huo, ambapo washindi walituzwa kupitia mchakato wa wazi na shirikishi.

Waziri pia alitangaza kuwa NYOTA itazinduliwa kikamilifu wakati wa Wiki ya Kimataifa ya Vijana mwezi Agosti, akisema kuwa kufikia wakati huo, waombaji wengi watakuwa wameidhinishwa kupokea msaada.

Kwa upande wake, Fikirini alikubaliana na kauli ya Waziri na kuwataka vijana kutumia ipasavyo fursa zilizopo.

"Huu ni wito wa kuchukua hatua. Kwa sasa tunapokea maombi ya mpango wa On-Job Experience (OJE) kupitia *254#, hivyo nawahimiza vijana wote kutuma maombi kwa vipengele vilivyofunguliwa pekee ili kuepuka makosa," alishauri.

Katibu huyo alisisitiza kuwa NYOTA pia inalenga vijana walio katika mazingira magumu wasiokuwa na sifa za kitaaluma, kwa kuwapa nafasi kupitia mfumo wa kutambua maarifa ya awali na vyeti vya kitaifa.

Aliongeza kuwa biashara za kijamii, upatikanaji wa zabuni za serikali, na programu za ujumuishaji wa kifedha vimejumuishwa katika mpango wa NYOTA ili kuwafikia vijana waliotengwa.

> Huu ni wito wa kuchukua hatua, tunakubali maombi chini ya mpango wa OJE

Fikirini alibainisha kuwa serikali inaendelea kujitolea kusaidia vijana kupata ajira za kimataifa kupitia Mpango wa Uhamaji wa Kazi (Labour Mobility Program), unaoongwa mkono na Hazina ya Uwezeshaji wa Vijana (YEDF).

"Idara ya Serikali kwa sasa inasaidia vijana 600, kila mmoja akipata hadi Sh300,000, ili waweze kuchukua nafasi za ajira nje ya nchi, na tumejikita kuhakikisha hakuna kijana anayebaki nyuma kwa sababu ya ukosefu wa msaada," alisema.

Fikirini pia alitaja kuwa fedha za kigeni kutoka kwa vijana wa Kenya wanaofanya kazi nje ya nchi kupitia mpango huo zilichangia zaidi ya Shilingi bilioni 5 kwenye uchumi mwaka jana.

Ili kuboresha upatikanaji wa huduma kwa vijana, Katibu huyo alitangaza kutengenezwa kwa "Youth Opportunity Passport" ya kidijitali, itakayojumuisha programu zote za serikali kwa vijana katika jukwaa moja.

Alitoa wito kwa Baraza la Taifa la Vijana kuharakisha mchakato wa kidijitali ili kuwezesha masasisho ya wakati halisi.

REPUBLIC OF KENYA

## PUBLIC SERVICE COMMISSION

**Our Vision**
"A citizen-centric public service"

**Our Mission**
"To reform and transform the public service for efficient and effective service delivery"

## PROFICIENCY EXAMINATION FOR CLERICAL OFFICERS- SEPTEMBER, 2025

It is notified for general information that year 2025 Proficiency Examination for Clerical Officers will be held from Monday 22nd to Thursday 25th September 2025 at Machakos; Nyeri; Mombasa; Embu; Garissa; Kisumu; Nakuru; Kakamega and Eldoret examination centers. The actual venues will be notified to the candidates after registration.

### ELIGIBILITY FOR REGISTRATION

To register for the Proficiency Examination for Clerical Officers, an officer must:

(a) Have passed the Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E.) with a mean grade of C – (minus) or its equivalent;
(b) Be designated as a clerical officer in the Public Service; and
(c) Have served as a clerical officer for a minimum period of one (1) year.

### REGISTRATION FORMS

**1. REGISTRATION FORMS**

(a) All candidates attempting the examination for the first time are required to complete registration FORM A while referred candidates should complete FORM B available on the Public Service Commission website **www.publicservice.go.ke**.

(b) The Candidate should submit the duly completed registration form, accompanied by the Government copy of the receipt generated from E-citizen platform to the Secretary/Chief Executive, Public Service Commission **P. O. Box 30095-00100 NAIROBI** so as to reach the Commission not later than **Friday, 22nd August, 2025.**

### REGISTRATION FEES

Each candidate will be required to pay registration fees as per the revised rates in the circular Ref **PSC. EXAM/1/VOL.11 dated 3rd May 2018.**

| | |
|---|---|
| **Basic Fee** | **Kshs. 2625** |
| **Fee per paper** | **Kshs. 875 (7 papers)** |
| **E-citizen fee** | **Kshs. 50** |

Candidates are required to pay the registration fee through the E-Citizen platform using the following procedure:

i. Log in to **https://psc.ecitizen.go.ke;**
ii. Select PSC Examinations;
iii. Click the apply now button;
iv. Log in to the e-citizen using your personal account;
v. Read the requirements for registration and click the next button;
vi. The applicants details will be uploaded from your personal e-citizen account;
vii. Click the next button;
viii. Select whether registering for the first time or for a re-sit;
ix. Select the type of examination;
x. For candidates who are re-sitting select the appropriate subjects;
xi. Select the examination center;
xii. Click the next button to preview the applicants details;
xiii. Click the next button to preview the examination details;
xiv. Click the next button and confirm that the information provided is accurate;
xv. Scroll to the bottom of the page and click the complete button;
xvi. Await approval from the Public Service Commission;
xvii. The approval status will be displayed on the applicant's E-citizen profile and communicated to their registered telephone number via SMS;
xviii. Once approval is granted, scroll back to your profile and click on the awaiting payment button;
xix. Make the payment through one of the gateways provided; and
xx. Download the Government copy of the receipt and attach it to the duly filled registration form.

### LATE REGISTRATION

A late registration fee of Kshs. 525 will be charged on all candidates who submit their registration forms after 22nd August, 2025. The deadline for late registration is **29th August, 2025.**

### COLLECTION OF CERTIFICATES

The certificates for candidates who passed the Proficiency Examination for Clerical Officers held in September 2024 are ready for collection at the Public Service Commission House during official working hours. Officers are requested to carry their original identification document. Officers who passed promotional examinations administered by the Public Service Commission in earlier years and have not collected their certificates are requested to do so.

This information can also be downloaded from the Public Service Commission website at **www.publicservice.go.ke.**

**PAUL FAMBA, MBS**
**SECRETARY/CEO**

KENYA VISION 2030

# SHA yafikia usajili wa milioni 24.8 huku TAIFA Care ikizidi kushika kasi

NA VICTOR KIPLAGAT NA KAMAU DANIEL (KNA)




**Waziri wa Afya Aden Duale alipokuwa akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kuhusu hatua muhimu za Mamlaka ya Afya ya Jamii (SHA) na Suala la Mafunzo ya Uuguzi. Picha na Daniel Kamau**

Wakenya takriban milioni 24.8 wamejiandikisha katika Mamlaka ya Afya ya Jamii (SHA), hatua kubwa inayohusishwa na kampeni kabambe za usajili katika kila kaunti.

Waziri wa Afya Aden Duale amepongeza mafanikio ya mageuzi ya SHA tangu kuzinduliwa kwa TAIFA Care mnamo Oktoba 1, 2024.

“Tunaelekea Nakuru kuendeleza kasi hii ili kuhakikisha hakuna Mkenya anayeachwa nyuma,” alisema wakati wa mkutano na wanahabari, huku akisisitiza umuhimu wa michango kutolewa kwa wakati ili kudumisha Mfuko huo.

Kulingana na Duale, Wakenya milioni 4.5 tayari wamepata matibabu kwa magonjwa ya kawaida na huduma za afya ya uzazi kupitia sehemu ya huduma za msingi, huku milioni 2.2 wakinufaika na huduma maalum — wakiwemo wagonjwa 8,000 waliopata huduma ya usafishaji figo na 18,000 waliopokea matibabu ya saratani.

Waziri huyo aliongeza kuwa huduma ya afya ya uzazi imesaidia zaidi ya akina mama 515,000 kujifungua tangu Oktoba 2024.

Hadi sasa, SHA imelipa Shilingi bilioni 6.8 kwa madai ya huduma za afya ya msingi, huku Shilingi bilioni 1.5 zikiwa tayari kutolewa.

“Tunalenga kuimarisha uthibitishaji na usindikaji wa madai ili kuhakikisha fedha zinatumika kwa uwazi na madai halali pekee ndiyo yanayolipwa,” alisisitiza.

Waziri huyo aliwahimiza Wakenya kuripoti malipo haramu katika vituo vya serikali, akieleza kuwa Sh 13b zimetengwa kufadhili huduma za afya ya msingi bila malipo, hasa katika vituo vya kiwango cha Pili hadi cha Nne.

Duale alifichua kuwa tayari amepokea ripoti kutoka kwa kamati huru inayochunguza upasuaji wa figo na ulanguzi wa viungo vya binadamu.

“Ni hati ya umma, na nawahimiza wanahabari kuichambua. Inazungumzia mapungufu ya kisheria, kiadili na kiafya, na pia inapendekeza mageuzi yanayoweza kutekelezwa,” alisema.

Aliahidi kuwasilisha matokeo hayo kwa Bunge na Baraza la Mawaziri, na kuongeza kuwa ripoti hiyo itatekelezwa kikamilifu.

Duale aliwahimiza Wakenya kuwa na subira kwa mchakato wa mageuzi unaoendelea.

“Tunajenga mfumo unaoleta usawa, uwajibikaji na huduma za afya kwa wote. Lengo letu ni uadilifu, ubunifu na utoaji bora wa huduma,” alisema.

Aliwataka wagonjwa walio na malalamiko kutumia Nambari ya Simu ya Dharura ya Wizara ya Afya (107 au 147) kupata msaada.

---

KNBS KENYA NATIONAL BUREAU OF STATISTICS *Keeping you informed* | fsd Kenya | Central Bank of Kenya

## 2025 REMITTANCES HOUSEHOLD SURVEY

The Kenya National Bureau of Statistics (KNBS), in collaboration with the Central Bank of Kenya (CBK) and Financial Sector Deepening Kenya (FSD Kenya), is conducting the first ever Remittances Household Survey (RHS) from July to September 2025.

Remittances represent international transfers in monetary (cash), and non-monetary (non-cash/in-kind) form sent by family members, friends and relatives living abroad to households in Kenya (inward remittances) or sent by households in Kenya to family members, friends and relatives living abroad (outward remittances). The remittances can be transferred through formal channels such as the banking system, couriers, money transfer operators, and mobile money or informal channels such as physically carrying across borders.

### Purpose

The purpose of the 2025 RHS is to collect qualitative and quantitative information on inward and outward remittances. The data collected will be used to improve national statistics for planning, research and policy formulation, including those related to supporting the remittance flows.

### Objectives

The overall objective of the 2025 RHS is to collect information on the amount of inward and outward remittances in Kenya. Specifically, the survey seeks to:

- Collect information on the amount of inward and outward remittances in cash and in-kind/non-cash.
- Establish the channels for remitting the transfers, the costs incurred, and the challenges faced.
- Establish the uses of remittances received to estimate the impact on the livelihood of the recipients.
- The difficulties encountered in sending or receiving money or in-kind/non-cash transfers.
- Provide policy recommendations for improving the remittances market in Kenya.

### Use of Data Collected

The 2025 RHS is expected to produce national estimates on the magnitude of remittance flows into Kenya and out of Kenya, both money and non-cash. The data collected from the 2025 RHS will be used for compilation of Balance of Payments statistics, monitoring Sustainable Development Goals (SDGs), research and policy formulation.

### Target Respondents

2025 RHS will be administered to households in Kenya who have received and/or sent remittances.

### Authority

The Statistics Act, CAP 112 Laws of Kenya [Rev. 2022] empowers KNBS to collect Remittance Statistics in Kenya, among other statistics. Households are legally bound to provide the required information.

### Confidentiality

Confidentiality of statistical information provided is guaranteed under the Statistics Act, CAP 112 Laws of Kenya [Rev. 2022] which can be accessed on the KNBS Website (***www.knbs.or.ke***). All the information provided will be treated with utmost confidentiality and will only be used for statistical purposes. The 2025 RHS personnel are under oath not to divulge information provided by the households to a third party.

### Output

The findings will be published in aggregated form on the KNBS, CBK and FSD Kenya websites.

### Appeal

The 2025 RHS Field Personnel will visit selected households during the survey period, which will be conducted, between **July and September 2025**. The Field Personnel will have identification badges. Given the importance of this exercise, we appeal to the selected households to cooperate and support the survey field staff.

We appreciate the continued cooperation and support in the production of official statistics.

| | | |
|---|---|---|
| Macdonald G. Obudho, PhD, EBS, MBS<br>Director General,<br>Kenya National Bureau of Statistics<br>Tel No: 020-2911000/1<br>Email:<br>directorgeneral@knbs.or.ke | Ms. Tamara Cook<br>Chief Executive Officer,<br>FSD Kenya<br>Tel No:+254 (20) 513 7300<br>Email:<br>info@fsdkenya.org | Dr. Kamau Thugge, CBS<br>Governor,<br>Central Bank of Kenya<br>Tel No: 020-2863200/3210<br>Email:<br>researchstat@centralbank.go.ke |

---

REPUBLIC OF KENYA

KENYA POWER PENSION FUND

## CAREER OPPORTUNITIES

Kenya Power Pension Fund (KPPF) is a Retirement Benefits Scheme registered with Retirement Benefits Authority, responsible for providing pension benefits to permanent and pensionable employees of Kenya Power and Nuclear Power & Energy Agency upon their retirement or withdrawal and to their dependents in the event of death in service.

In pursuing its mandate, KPPF is seeking to recruit top talents to join the innovative and transformative team to deliver on key milestones of the Fund. The individuals who will fill this position should be result oriented, self-driven, creative, visionary and of high integrity.

Applications are therefore invited from qualified persons to fill the vacancy indicated in the matrix below:

| No. | Job Title | Ref No. | No. of Vacancies |
|---|---|---|---|
| 1 | Manager, Planning & Strategy - **Re-advertisement** | KPPF/HRA-HR/1/25/7 | 1 |

**How to Apply**

Interested and qualified candidates are advised to visit the Fund's website for detailed job descriptions for the roles at **www.kppf.co.ke/careers/**. Applications should be sub-mitted through the link: **https://e-recruitment.kppf.co.ke** to be received not later than **Tuesday 12th August, 2025.**

Canvassing will lead to disqualification.

KPPF is an equal opportunity employer. Marginalized groups and persons living with disabilities are encouraged to apply. Only shortlisted candidates will be contacted.

**The CEO & Trust Secretary**
**Kenya Power Pension Fund**
**P.O Box 1548 00600 Nairobi**

KENYA VISION 2030

# Mitaa ya mabanda Nakuru kufanyiwa ukarabati mkubwa wa miundombinu

NA ESTHER MWANGI NA MARY OCHIENG, KNA

Katika vitongoji vya Jiji la Nakuru, mabadiliko ya kimya yanaendelea. Makazi manne yasiyo rasmi—ambayo hapo awali yalijulikana kwa uhalifu, usafi duni, mifumo ya mifereji iliyoziba, na barabara zilizoharibika—sasa yanabadilika polepole lakini kwa hakika. Kwa miongo kadhaa, makazi haya pia yalijulikana kama maeneo hatarishi kwa magonjwa yanayosababishwa na maji, yakiwemo kipindupindu na homa ya matumbo. Hata hivyo, baada ya miaka mingi ya kuishi katika mazingira duni, sura mpya inaanza kuchomoza kwa wakazi wa Kwa-Murogi, London-Hilton, na Lake View katika Mji wa Nakuru, pamoja na mitaa ya mabanda ya Karagita huko Naivasha—maeneo ambayo zamani yalitambulika kwa njia nyembamba na huduma finyu. Mradi wa Uboreshaji wa Makazi Yasiyo Rasmi wa Kenya (KISIP 2) unaleta mageuzi katika jamii hizi, ukileta matumaini, usalama, na fursa kwa mamia ya maelfu ya wakazi, hasa katika mitaa ya mabanda inayojulikana ya Kaunti ya Nakuru. Idara ya Serikali ya Nyumba na Maendeleo ya Miji, kupitia KISIP 2 inayofadhiliwa na Benki ya Dunia, imewekeza Shilingi bilioni 1.5 kuboresha makazi yasiyo rasmi. Mpango huu umefanikiwa kwa kiwango kikubwa katika kuboresha upatikanaji wa huduma za msingi, kuimarisha umiliki wa ardhi, na kuimarisha mifumo ya taasisi kwa ajili ya uboreshaji wa mitaa ya mabanda katika mfumo wa ugatuzi. Alex Wachiuri, mkazi wa Kwa-Murogi katika Eneo Bunge la Nakuru Mashariki tangu mwaka 1974, alielezea historia ya eneo hilo kuwa ya kusikitisha, akisema kuwa wawekezaji waliepuka eneo hilo kutokana na ukosefu wa miundombinu na huduma muhimu za kuendesha biashara. Aliongeza kuwa mfumo wa maji taka haukuwa wa kuridhisha, na taka kutoka vyooni zilikuwa zikipenya hadi ndani ya nyumba, kando ya barabara, vyanzo vya maji, na masoko. “Eneo hili lilijaa harufu ya pombe haramu na uchafu, na lilikuwa kitovu cha magonjwa. Hakuna mtu aliyependa kuishi hapa,” alisema.



Sehemu ya wafanyikazi wanaohusika katika mradi wa KISIP 2 katika makazi ya Lakeview huko Nakuru.

Wachiuri alieleza zaidi kuwa kadri idadi ya watu ilivyoongezeka, hali ya usalama ilidorora, na hivyo wakazi kulazimika kuandamana na kudai kujengwa kwa kituo cha polisi karibu. Hata hivyo, tangu Machi mwaka huu, dereva wa zamani wa matatu mwenye umri wa miaka 73 ameona mabadiliko chanya kufuatia uzinduzi wa mradi wa KISIP 2. Wawekezaji binafsi wameanza kujenga majengo ya makazi na biashara katika eneo hilo. KISIP ulianzishwa na serikali mwaka 2011 kwa usaidizi kutoka Benki ya Dunia, Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Uswidi (Sida), na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD). Miradi ya uboreshaji wa mitaa ya mabanda inatarajiwa kukamilika ifikapo mwaka 2027. Kwa sasa, Kwa-Murogi ipo katika Awamu ya Pili ya uboreshaji kupitia KISIP, ambayo inajumuisha ujenzi wa barabara.

# Mamlaka yasambaza mbuzi 1,000 aina ya Galla kwa familia maskini Baringo



**Afisa Mkuu Mtendaji wa Mamlaka ya Kitaifa ya Kukabiliana na Ukame Hared Adan anaungana na viongozi wengine wa Baringo kusambaza pesa za Galla 500 kwa familia zenye mahitaji katika eneo la Chebarsiat katika Wadi ya Saimo Soi, Baringo Kaskazini Jumanne.**

NA BENSON KELIO NA JOSHUA KIBET (KNA)

Mamlaka ya Kitaifa ya Kudhibiti Ukame (NDMA) imeanza kusambaza mbuzi wa kiume wa Galla 1,000 katika eneo la Baringo Kaskazini kama njia ya kurejesha maisha ya familia zilizoathiriwa na ukosefu wa usalama. Akizungumza baada ya kuzindua zoezi hilo katika eneo la Chebarsiat, Afisa Mtendaji Mkuu wa NDMA, Hared Adan, alisema mamlaka hiyo inashirikiana na Serikali ya Kaunti ya Baringo kupitia Mfuko wa Dharura wa Kitaifa wa Ukame (NDEF), kufuatia ombi la wakazi wa Wadi ya Saimo Soi, miaka mitatu iliyopita. Adan, aliyekuwa ameandamana na Naibu Gavana wa Baringo, Mhandisi Felix Kimaiyo, pamoja na Mbunge wa eneo hilo Joseph Makilap, alisambaza mbuzi wa Galla 500 kwa ajili ya eneo la Bartum. Alisema mbuzi wengine 500 wanasubiri kusambazwa kwa wakazi wa maeneo ya Sibilo na Yatya. Afisa huyo alisema kuwa mamlaka hiyo pia imepata ufadhili wa kusaidia wakazi wa Tiaty kwa kuwapatia ngamia 500 watakaowasili katika kipindi cha wiki tatu zijazo. “Lengo letu kuu ni kusaidia jamii zote katika maeneo kame na yenye ukame kwa kuinua maisha yao,” alisema Adan. Alifichua kuwa Kaunti ya Baringo pia imejumuishwa katika awamu ya pili ya mpango wa uhawilishaji wa fedha wa Mradi wa Kijamii na Kiuchumi wa Ujumuishaji wa Kenya (KSEIP), unaotarajiwa kuanza kutekelezwa katika miezi michache ijayo baada ya kuwatambua walengwa. Naibu Gavana, katika hotuba yake, aliisifu mamlaka hiyo kwa msaada mkubwa ambao alisema utasaidia kuboresha mifugo wa kienyeji kwa matumizi ya nyumbani na soko la nje. Mhandisi Kimaiyo alieleza kuwa mpango huo umefika kwa wakati mwafaka kwani utasaidia machinjio ya Maoi iliyoko Baringo Kusini ambayo iko katika hatua za mwisho kukamilika, na ambayo inahitaji mifugo 1,000 kwa siku ili kufanya kazi kwa ufanisi.


REPUBLIC OF KENYA

**MINISTRY OF EDUCATION**

***STATE DEPARTMENT FOR TECHNICAL & VOCATIONAL EDUCATION & TRAINING***

AFRICAN DEVELOPMENT BANK GROUP

## SPECIFIC PROCUREMENT NOTICE

## ADDENDUM 1

| | |
|---|---|
| **PURCHASER** | MINISTRY OF EDUCATION \| STATE DEPARTMENT FOR TECHNICAL, VOCATIONAL EDUCATION & TRAINING |
| **PROJECT** | SUPPORT TO TECHNICAL AND VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AND ENTREPRENEURSHIP (TVETE) PROJECT – (GOK/AFDB TVET PHASE III PROJECT) |
| **COUNTRY** | KENYA |
| **DATE** | 29TH JULY 2025 |
| **LOAN NO.** | ADF No. 2100150042254 |
| **SUBJECT** | ADDENDUM NUMBER 1 |

This addendum Number 1 relates to the Specific Procurement Notice (SPN) for the tender for Supply, Installation, Calibration, Commissioning and Training on the Use and Maintenance of training equipment as shown below:

| | OCBI NO. | TENDER DESCRIPTION |
|---|---|---|
| 1 | OCBI/TVETE PHASE III/EQUIP/47/24-25 | Lot 1 - Tender for Supply, Installation, Calibration, Commissioning and Training on the use and Maintenance of Building and Civil Engineering Training Equipment |
| 2 | OCBI/TVETE PHASE III/EQUIP/48/24-25 | Lot 2 - Tender for Supply, Installation, Calibration, Commissioning and Training on the use and Maintenance of Mechanical & Automotive Engineering Training Equipment |
| 3 | OCBI/TVETE PHASE III/EQUIP/49/24-25 | Lot 3 - Tender for Supply, Installation, Calibration, Commissioning and Training on the use and Maintenance of Hospitality and Tourism Training Equipment and Assistive Training Equipment |
| 4 | OCBI/TVETE PHASE III/EQUIP/50/24-25 | Lot 4 - Tender for Supply, Installation, Calibration, Commissioning and Training on the use and Maintenance of Printing and Publishing Equipment |

The tender appeared in the **Star Newspaper – My Gov pull out**, the Ministry of Education (Kenya) and the African Development Bank websites and the UNDB online on **17th June 2025,** and prospective bidders are advised as follows:

1. That the closing/opening date has been extended from **Thursday, 7th August 2025 to Thursday 21st August 2025** to give adequate time to bidders to prepare bids incorporating clarifications to questions raised.
2. That all the other conditions and Instructions to Bidders shall remain as in the tender documents and initial Specific Procurement Notice.
3. That all subsequent addendums shall be published on the Ministry of Education website **www.education.go.ke** and African Development Bank (AfDB) website: **www.afdb.org** and shall form part of the final submission. This will be taken into account in the evaluation and selection of the successful bidders.

**HEAD – SUPPLY CHAIN MANAGEMENT SERVICES**
**FOR: PRINCIPAL SECRETARY**

# Wito umma ushiriki kuteua mashujaa kabla ya Mashujaa Dei

NAIMMACULATE CHEBET
(MYGOV)

Baraza la Kitaifa la Mashujaa (NHC) kwa sasa linapokea mapendekezo ya watu wanaostahili kutambuliwa kama mashujaa wa taifa nchini Kenya, watakaotuzwa wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Mashujaa mwaka huu. Kulingana na Afisa Mkuu Mtendaji wa NHC, Charles Wambia, “Mapendekezo yanaweza kutolewa na umma, kaunti, mashirika, vikundi au taasisi. Mwisho wa kuwasilisha mapendekezo ni tarehe 31 Julai 2025.” Wambia alisema kuwa waliopendekezwa wanapaswa kuwa wameonesha utumishi wa kipekee kwa taifa katika mojawapo ya maeneo 14 ya kiutendaji yaliyoainishwa kwenye Sheria ya Mashujaa ya Kenya. “Maeneo haya ni pamoja na harakati za ukombozi, uongozi wa kiroho, maarifa asilia, maadili na tamaduni za kitamaduni, sanaa, michezo, utafiti na taaluma, taaluma na utafiti, upatanishi wa amani, uongozi wa kitaifa, ujasiriamali na sekta ya viwanda, ufadhili, haki za binadamu, mshikamano na muungano wa kitaifa, na uhifadhi wa mazingira,” alisema Mkurugenzi huyo. Alihimiza umma kuhakikisha kuwa vitendo vya wanaopendekezwa vinaendana na maadili yaliyoainishwa katika Ibara ya 10 ya Katiba ya Kenya kama vile ushujaa, nidhamu, kujitolea, na uvumilivu. “Fomu ya mapendekezo pamoja na nyaraka za kuunga mkono inaweza kuwasilishwa kwa barua pepe, kwa posta, au kwa kuwasilishwa moja kwa moja katika ofisi za NHC,” aliongeza.

Katika ziara hiyo, Wambia alikiri urithi wa Mzee Meza na kusisitiza umuhimu wa kutambua raia waliosaidia kuunda historia ya Kenya. Aidha, alisisitiza wito unaoendelea wa kuwasilisha mapendekezo, akiwahimiza Wakenya kuwasilisha majina ya watu ambao matendo yao yameleta mabadiliko ya kipekee kwa taifa. “Ili mtu atambuliwe kama shujaa, lazima awe amejitolea bila kujali maslahi yake binafsi na kutoa sadaka kwa ajili ya taifa. Lazima waonyeshe wazi athari ya kazi yao kwa watu au jamii, iwe ndani ya nchi au kimataifa,” alisema Afisa Mkuu Mtendaji wa Baraza hilo. Alieleza kuwa mapendekezo yanayowasilishwa yanapaswa kuambatana na fomu iliyojazwa inayoonyesha kazi ya mtu anayepewa mapendekezo, viungo vya tovuti vinavyoonyesha kazi yao au makala kuhusu wao endapo zinapatikana. Pia yanapaswa kuambatana na nakala za picha zinazoonyesha kazi yao, barua za mapendekezo, barua za pongezi au shukrani kutoka kwa jamii au watu walioguswa na kazi ya shujaa huyo, nakala za makala ya magazetini..




**Mtoto wa Marehemu Mzee Meza Morowa Galana, Hiribae Rodgers (katikati) alipotembelea ofisi za Baraza la Mashujaa Taifa. Mzee Meza alitunukiwa baada ya kifo chake kwa mchango wake katika utunzi wa Wimbo wa Kitaifa wa Kenya. Kushoto ni Mwenyekiti wa Baraza hilo Jimmy Angwenyi akiwa na Mkurugenzi Mtendaji Charles Wambia.**

REPUBLIC OF KENYA

## MINISTRY OF ROADS AND TRANSPORT

### STATE DEPARTMENT FOR ROADS

### JOB ADVERTISEMENT

Applications are invited from qualified persons for the following positions shown below:

| VACANCY NO | JOB TITLE | CSG | POSTS |
|---|---|---|---|
| 2/2025 | Housekeeping Assistant I | 13 | 3 |
| 3/2025 | Driver Instructor III KIHBT | 13 | 7 |
| 4/2025 | Plant Operator Instructor III KIHBT | 13 | 8 |
| 5/2025 | Housekeeping Assistant III | 15 | 27 |
| 6/2025 | Cook III | 15 | 23 |
| 7/2025 | Waiter Assistant III | 15 | 5 |
| 8/2025 | Artisan III (General Power Electrician) | 15 | 3 |
| 9/2025 | Artisan Tailoring III | 15 | 3 |
| 10/2025 | Artisan Auto Electrician Mechanic III | 15 | 15 |
| 11/2025 | Artisan Motor Vehicle Mechanic III | 15 | 10 |
| 12/2025 | Artisan Mechanical III | 15 | 6 |
| 13/2025 | Artisan Building III | 15 | 4 |
| 14/2025 | Artisan Plant Mechanic III | 15 | 16 |
| 15/2025 | Artisan Spray Painter III | 15 | 4 |
| 16/2025 | Artisan Panel Beater III | 15 | 5 |
| 17/2025 | Artisan Upholster III | 15 | 4 |
| 18/2025 | Plant Operator III | 15 | 11 |
| 19/2025 | Driver II (Light & Heavy Commercial | 15 | 12 |
| 20/2025 | Security Warden III | 15 | 23 |

Interested and qualified persons are requested to make their applications by completing one PSC2 *(Revised 2016)* application form. The form may be downloaded from the Public Service Commission's websites: **www.publicservice.go.ke**

For more details on salary scale, requirements for appointment, duties and responsibilities, visit the following website **www.roads.go.ke.**

Completed PSC 2 (2016) application form can be sent to: -

**The Principal Secretary**
**State Department for Roads**
**Ministry of Roads and Transport**
**P.O. Box 30260-00100 Nairobi**

**OR**

Hand delivered to the **State Department for Roads Human Resource Management registry, Transcom House, 5th Floor** on or before **22nd August, 2025.**

REPUBLIC OF KENYA

KeNHA Kenya National Highways Authority
Quality Highways, Better Connections

### CAREER OPPORTUNITY

The Kenya National Highways Authority (KeNHA), a State Corporation under the Ministry of Roads and Transport was established under the Kenya Roads Act, 2007 and charged with the mandate to manage, develop, rehabilitate, and maintain national trunk roads.

To carry out this mandate effectively, the Authority wishes to fill the following vacant position with creative and proactive Kenyan citizens with the ability to quickly adapt to a dynamic work environment.

| No. | Job Title | KeNHA Grade | Reference Number | Position |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Director, Internal Audit | 2 | KeNHA/D-IA/01/2025 | 1 |

All candidates who meet the requirements detailed in the Job Specifications should apply using the provided email **boardrecruitement@kenha.co.ke** or through the specific address shown below by close of business on **Monday, 18th August 2025 at 5:00 pm.**

For a detailed Job Profile and Specification, and general information on KeNHA, please visit the Authority's website **www.kenha.co.ke**.

KeNHA is an Equal Opportunity Employer committed to diversity and gender equality within the organization and therefore encourages persons with disability, women and those from marginalized areas to apply. Applicants with disability are requested to indicate their status on the application link for ease of identification.

Prospective candidates **MUST** satisfy the requirements of Leadership and Integrity set out in Chapter six (6) of the Constitution of Kenya and shall be required to present the following documents during the interview.
- Ethics and Anti-corruption Commission Clearance Certificate
- Kenya Revenue Authority Tax Compliance Certificate
- Higher Education Loans Board Clearance Certificate or proof of ongoing repayments
- Certificate of Good Conduct issued by National Police Service
- Certificate of Clearance from the Credit Reference Bureau (CRB) The above documents will not be required at the point of application.

The terms of appointment for the above positions shall be on a five (5) year Contract Terms of Service:

Applications for the position should be addressed to: -

**The Chairperson, Board of Directors,**
**Kenya National Highways Authority,**
**Barabara Plaza, Jomo Kenyatta International Airport (JKIA)**
**Off Airport South Road, along Mazao Road**
**P.O. Box 49712 - 00100 Nairobi.**

Applications **clearly quoting the reference number** should be hand delivered and inserted in the **Recruitment box** placed at **4th Floor** (*Outside the Director General's Office*).

Applications without the relevant qualifications will not be considered. Any form of canvassing shall lead to automatic disqualification.

***Only shortlisted candidates will be contacted.***

**Vision:** A quality National Trunk Road Network to all for prosperity
**Mission:** To develop and manage resilient, safe, and adequate National Trunk Roads for sustainable development through innovation and optimal utilization of resources
Core Values: Accountability | Sustainability | Innovation | Teamwork

@KeNHAKenya | Kenya National Highways Authority | KeNHA TV | Kenya National Highways Authority | kenha_kenya | @kenhaofficial

ISO 9001 : 2015 & ISO/IEC 27001 : 2022 Certified

# Serikali kuondoa Sh6b kwa riba ili kuachilia maelfu ya hati miliki



**Waziri wa Ardhi na Mipango ya Miji, Alice Wahome, akihutubia wananchi wakati wa uzinduzi rasmi wa Masjala ya Ardhi.** PICHA: SHANI RHAI

**NA EMMANUEL MASHA AND SHANI RHAI, KNA**

Wizara ya Ardhi inapanga kufutilia mbali riba ya zaidi ya Shilingi bilioni 6 kwenye ada za makazi ambazo hazijalipwa, ili kusaidia walionufaika na mgao wa ardhi kuchukua hatimiliki ambazo hazijadaiwa kote nchini, Waziri wa Ardhi Bi. Alice Wahome amefichua.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Ofisi ya Ardhi ya Malindi, Bi. Wahome alisema tayari ameandaa waraka wa baraza la mawaziri na kuupeleka kwa Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Fedha.

"Nimetuma ombi kwa Waziri wa Hazina. Pia tumelizungumzia suala hili na Rais ili, tukubaliana, tuweze kufuta riba hiyo," alisema, na kuongeza kuwa, "nina waraka wa baraza la mawaziri ambao uko kwa Mwanasheria Mkuu na Waziri wa Fedha."

Ni wakati wa kihistoria kwa Kenya. Hewa imejaa msisimko huku nchi ikijiandaa kwa mara ya kwanza kuandaa Mashindano ya Mataifa ya Afrika (CHAN) ya Shirikisho la Soka Barani Afrika (CAF). Kenya itakuwa mwenyeji wa mechi za siku ya pili kati ya timu ya taifa ya Harambee Stars na timu ya taifa ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DR Congo) katika Uwanja wa Kimataifa wa Michezo wa Moi, Kasarani, Jumapili tarehe 3 Agosti saa 9:00 alasiri (15:00 EAT / 12:00 GMT). CHAN, ambayo inaandaliwa kwa pamoja na Tanzania na Uganda, itaanza tarehe 2 Agosti na kukamilika tarehe 30 Agosti 2025. Tanzania itakuwa mwenyeji wa mechi ya ufunguzi kati yake na Burkina Faso katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam. Fainali ya mashindano hayo yatafanyika Kenya, huku Uganda ikipanga mechi ya mchujo wa nafasi ya tatu katika Uwanja wa Mandela jijini Kampala. Waziri wa Masuala ya Vijana, Uchumi wa Ubunifu na Michezo, Salim Mvurya, alithibitisha kuwa Kenya iko tayari kuandaa mechi hizo baada ya kikao cha juu na ujumbe wa CAF. Ujumbe huo uliwajumuisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Michezo Elijah Mwangi, Rais wa FKF Hussein Mohammed, na Mwenyekiti wa Kamati ya Maandalizi ya Mashindano hayo nchini, Nicholas Musonye. "Tuko tayari kuandaa CHAN 2024. Kila jambo lililotakiwa kutoka kwetu limefanyika, na CAF imethibitisha kuwa tuko kwenye njia nzuri," alisema Mvurya. Usalama umeimarishwa, huku Waziri huyo akisisitiza dhamira ya serikali kuhakikisha tukio hilo linafanyika kwa mafanikio makubwa. Ameeleza kuwa mashindano hayo ni "fursa kubwa" kwa Kenya, akirejelea nafasi zilizopotea za kuandaa matukio makubwa mwaka 1996 na 2018. Pia alitoa shukrani kwa Rais wa CAF Patrice Motsepe kwa msaada na mwongozo wake wa kudumu uliosaidia Kenya kufikia viwango vya kimataifa vya mashindano hayo. Katibu Mkuu wa CAF, Veron Mosengo-Omba, akizungumza baada ya kutembelea viwanja muhimu ikiwemo Uwanja wa Nyayo na Kasarani, alielezea kuridhishwa na maendeleo yaliyopatikana. "Kila kitu kipo tayari. Tuko tayari kwa mchezo wa ufunguzi tarehe 2 Agosti. Tukio hili ni jukwaa muhimu la kuonyesha ulimwengu kuwa Kenya ina uwezo wa kuandaa mashindano ya kimataifa, yakiwemo AFCON 2027," alisema Mosengo-Omba. Alisifu maandalizi yaliyofanyika, akibainisha kuwa miundombinu ya viwanja, hali ya nyasi, na maandalizi ya uendeshaji ni ya kiwango cha juu. Katibu huyo alisifu juhudi za kueneza taarifa na kuhamasisha umma kuhusu mashindano hayo


## KENYA INSTITUTE OF CURRICULUM DEVELOPMENT

*Nurturing Every Learner's Potential*

### ADDENDUM II TO THE INVITATION TO SUBMIT COURSE MATERIALS FOR EVALUATION AND APPROVAL

Reference is made to our advert and **Addendum in 'mygov' newspaper dated 20th May and 1st July 2025; respectively,** on Submission, Evaluation and Approval Procedures for Competency Based Curriculum (CBC) Support Materials for SENIOR SCHOOL 2025 Edition.

This is to inform all publishers and others interested in submitting curriculum support materials for evaluation and approval that:

**1.** The literary texts for Literature in English and Fasihi ya Kiswahili have been amended as follows:

| No. | LITERATURE IN ENGLISH | GRADE |
|---|---|---|
| 1 | Novel from Kenya | 10,11,12 |
| 2 | Autobiography | |
| 3 | Biography | |
| 4 | Anthology of short stories (including stories from Kenya, Africa and the rest of the World) | |
| 5 | Anthology of poetry (including poetry from Kenya, Africa and the rest of the World) | |
| 6 | Textbook on Oral Literature | |
| 7 | Textbook on Poetry | |
| | **KISWAHILI** | |
| 1 | Wasifu | 10,11,12 |
| 2 | Hadithi Fupi (hadithi thelathini katika kitabu kimoja) | |
| 3 | Kitabu cha Fasihi Simulizi | |
| 4 | Kitabu cha Mashairi | |

**NOTE:**

**For both literature and Fasihi**

- The Novel, Autobiography and Biography should be literarily rich in terms of context, plot, themes, characterization, aspects of style, length and language; **to sufficiently engage learners** who shall have opted for literature in English and Fasihi ya Kiswahili for the next four years.
- The plots, themes and structures of the texts in the anthologies of short stories and poetry should be varied and in tandem with the core competencies, values and Pertinent Contemporary Issues (PCIs) as outlined in the curriculum designs.
- The level of language in the literary texts MUST be appropriate to the learners in the grades 10, 11 and 12.
- The literary texts MUST also take cognisance of **relevance** to the age, academic level and psychosocial developmental level of the learners at Senior School and topicality in terms of social, economic, political develoments in Kenya, Africa and the World Currently.
- For Autobiography and Biography in particular, they should preferably be based on the Kenyan or African context; though texts from the rest of the world would also be acceptable if they show remarkable relevance.

**2.** The date of submissions has been changed from **6th August 2025 to 12th August 2025.** Submissions must be made by **12p.m, 12th August 2025.**

Curriculum support materials received will be opened/announced in the presence of submitting publishers who wish to attend at **12.30 p.m. on 12th August 2025 at the, KICD, Desai Road off Murang'a Road, Nairobi, KENYA.**

All other guidelines remain unchanged.

Any enquiries on submission of materials should be directed to:

**The Director/ Chief Executive Officer**
**Kenya Institute of Curriculum Development**
**P.O. Box 30231 – 00100 NAIROBI – Kenya**
**Tel: (254 020) 3749900 – 3, +254 729327334**
**E-mail: info@kicd.ac.ke or materialevaluation@kicd.ac.ke**

# Kaunti kumi na moja zatunukiwa kwa kutanguliza afya katika bajeti na ununuzi

**NA CHRISTINE CHERYL (MYGOV)**




**Mkurugenzi Mtendaji wa KEMSA, Dkt. Waqo Ejersa, akimkabidhi kombe Mfamasia wa Kaunti ya Kitui Dkt. Beatrice Muia, akisherehekea utendakazi bora wa kaunti katika usimamizi wa ugavi wa afya.**

Mamlaka ya Ugavi wa Dawa Kenya (KEMSA) inashirikiana na Wafamasia wa Kaunti pamoja na Idara ya Bidhaa na Teknolojia za Afya (DHPT) ili kulinganisha vipaumbele vya ugavi wa dawa na mahitaji halisi ya afya kwa wakati. KEMSA iliandaa warsha ya kitaifa ya kimkakati mjini Naivasha kwa lengo la kuharakisha mageuzi katika mfumo wa afya uliogatuliwa nchini Kenya, kusherehekea kaunti ambazo zimefanya vizuri katika kupanga kwa mkakati ugavi wa dawa kama sehemu kuu ya utoaji huduma za afya, na kuweka msingi wa mnyororo wa usambazaji wa huduma za afya unaotegemea takwimu. Hafla hiyo ilionyesha kaunti ambazo zimeweka afya katikati ya mipango yao kwa kutenga bajeti maalum kwa ajili ya Bidhaa na Teknolojia za Afya (HPT), kulipa madeni yao kwa KEMSA kwa wakati, na kulinganisha ununuzi wao na mahitaji mbalimbali ya kiafya ya watu wao kwa wakati halisi.

“Hii si mkutano mwingine tu — huu ni mwanzo mpya,” alisema Dkt. Waqo Ejersa, Mkurugenzi Mkuu wa KEMSA. “Tunabuni upya mifumo yetu, sera na ushirikiano ili kila shilingi ihesabike, kila bidhaa iwe na maana, na hakuna Mkenya abakie bila dawa anayohitaji. Enzi ya ununuzi wa kubahatisha imekwisha.”

Kama sehemu ya kaulimbiu ya warsha hiyo, “Kutoa Huduma kwa Umoja,” KEMSA ilitunuku kaunti kumi na moja kwa utendaji bora katika usimamizi wa HPT kwa mwaka wa fedha wa 2024-2025. Kaunti hizo ni pamoja na Machakos, Kitui, Elgeyo Marakwet, Turkana, Mandera, Kwale, Nyeri, Meru, Narok, Kisumu na Busia, ambazo zilitambuliwa kwa kuweka oda kwa wakati, usimamizi mzuri wa mikopo, na kuipa kipaumbele KEMSA kama msambazaji wao mkuu wa bidhaa za afya.

Vivyo hivyo, Wafamasia wa Kaunti kumi na sita walitambuliwa binafsi kwa uongozi bora katika usimamizi wa bidhaa za afya. Miongoni mwa waliotunukiwa ni Dkt. Alex Oindi (Machakos), Dkt. Beatrice Muia (Kitui), Dkt. Brian Muyokani (Turkana), Dkt. Jerusa Oluhano (Vihiga), Dkt. Kepher Mogere (Kisii), Dkt. Nancy Olunga (Siaya), na Dkt. Matthew Yegon (Bomet) kwa kujitolea kwao kuhakikisha ununuzi kwa wakati, usimamizi wa madeni, ushirikiano na wadau, na mikakati bunifu ya kuboresha matokeo ya usambazaji wa huduma za afya. Dhamira yao inaakisi juhudi za kitaifa za kujenga mfumo wa afya thabiti, wazi, na unaoangazia mahitaji ya watu.

“Tunajenga mnyororo wa usambazaji unaotegemea takwimu, si kubahatisha,” alieleza Dkt. Ejersa. “Mfumo wetu mpya wa ERP utabadilisha mrejesho kutoka vituo vya afya kuwa maarifa yanayoweza kutekelezwa. Hivi ndivyo tunavyokomesha upungufu wa dawa, kupunguza upotevu, na kurejesha imani katika mfumo wa afya wa umma.”

> Hii ni zaidi ya masanduku ya kusonga, mifumo na hisa. Inahusu kuokoa na kubadilisha maisha

Jukwaa hilo pia liliashiria hatua muhimu katika ajenda ya mabadiliko ya KEMSA, kufuatia wito wa Waziri wa Afya Aden Duale wa kuwa na mnyororo wa ugavi wa kisasa unaotegemea teknolojia. Dkt. Ejersa alibainisha kuwa kiini cha mabadiliko hayo ni uzinduzi wa mfumo mpya wa Enterprise Resource Planning (ERP) unaokusanya data ya mahitaji kutoka kwa vituo vya afya kote nchini kwa wakati halisi na kuongoza ununuzi sahihi wa bidhaa.

“Hii ni zaidi ya kuhamisha maboksi, mifumo na hisa. Hii ni kuhusu kuokoa na kubadili maisha,” alisisitiza Dkt. Ejersa. “Wakati Wafamasia wa Kaunti wanapotuambia wanachohitaji na tukachukua hatua haraka na kwa usahihi, tunawaokoa watu.”

Dkt. Ejersa pia alizitaka kaunti zilizo na madeni kwa KEMSA kulipa salio lao ili kuhakikisha ugavi usioingiliwa wa bidhaa muhimu za matibabu. Alihimiza kaunti zote kutumia Mamlaka ya Afya ya Jamii (SHA) ili kupanua upatikanaji wa huduma bora za afya kwa wote.

Akizingatia mtindo wa kibiashara wa KEMSA usio wa faida ambapo mapato yote yanawekezwa tena katika mfuko wa kitaifa wa mzunguko, Mkurugenzi Mkuu huyo alieleza kuwa changamoto za kifedha zimeilazimu Mamlaka kufikiria upya mtindo wake wa biashara kwa nia ya kuwa mnyumbufu, wa kisasa, na endelevu zaidi.

“Tunabadilisha gia,” alisema. “Lengo letu ni kufikia kiwango cha zaidi ya asilimia 90 cha kujaza oda kwa haraka iwezekanavyo.”

# Safari ya Miriam Chepchumba kutoka kijijini hadi kuwa mekanika tajika

**NA GILBERT MUTAI NA JOYCE JEPKOSGEI, KNA**



**Miriam Chepchumba akipumzika baada ya kurekebisha tairi la lori lililokuwa na hitilafu katika karakana yake.** PICHAJOYCE JEPKOSGEI

Akiwa na umri wa miaka 21 pekee, Miriam Chepchumba—mama wa mtoto mmoja na fundi magari aliyehitimu—anavunja mila na desturi zilizokita mizizi katika sekta ya magari inayotawaliwa na wanaume nchini Kenya.

Mikono yake iliyokunjamana kwa kazi inaelezea hadithi ya ustahimilivu ambayo inaendelea kuwatia moyo wasichana wengi.

Safari ya Chepchumba ilianza kwenye vilima vya Kericho, ambapo alipokuwa mtoto, alikuwa akitazama matrekta yakipita kwenye barabara za mashamba zilizoteremka kwa mwinuko.

“Wakati wengine walikuwa wakiziba masikio yao kutokana na kelele, mimi ningekaribia zaidi, nikivutiwa na jinsi mashine hizi zilivyoweza kushinda vilima ambavyo watu walishindwa kuvipanda,” alikumbuka.

Udadisi wake wa utotoni uligeuka kuwa ari ya kweli alipongalia kipindi cha runinga kuhusu fundi mwanamke huko Nairobi.

“Makala ile ilipanda mbegu. Kwa mara ya kwanza, niliona ushahidi wa wazi kuwa injini siyo jambo la wanaume pekee,” Chepchumba alisema.

Akiwa na miaka 17, akiwa hana chochote ila ari, alitembelea gereji za eneo lao akitafuta mafunzo kwa njia ya uanagenzi—lakini majibu aliyopata yalivunja moyo.

“Walinambia niende nikajifunze ususi badala yake,” alisimulia.

Mmiliki mmoja wa gereji hatimaye alikubali, lakini badala ya kumpa vifaa vya kazi, alimkabidhi ufagio na kusema, “Fagia kwanza, halafu tutaona.”

Kwa miezi sita, Miriam alifagia sakafu, kupanga vifaa, na kutazama mafundi wakifanya kazi wakati wa mapumziko yake.

Usiku, alisoma miongozo ya kutengeneza magari iliyotupwa kwa mwanga wa taa ya mafuta ya taa.

Bidii yake ilizaa matunda wakati pikipiki ya jirani yao ilipoharibika. Baada ya mafundi kadhaa kushindwa kuirekebisha, Miriam aliomba nafasi ya kuijaribu.

“Wote walicheka hadi nilipoonyesha tatizo lilikuwa kwenye carburetor,” alisema.

Ndani ya saa chache, injini ilikuwa inafanya kazi vizuri.

Habari zilienea haraka katika jamii yao ya karibu, na muda si muda wakazi walikuwa wakimletea vifaa vyao vilivyoharibika na baiskeli kwa “msichana anayerekebisha vitu.”

Hata hivyo, licha ya sifa zake kukua, Chepchumba alikumbana na changamoto nyingi ambazo wenzake wa kiume hawakuzipitia.

Wasambazaji walimtoza bei za juu wakidhani hajui bei sahihi. Wateja pia walifika gereji yake wakitaka kuzungumza na ‘fundi halisi’ na wengine walikataa kabisa kumruhusu afanye kazi kwenye magari yao hadi alipoonyesha ujuzi wake.

“Kulikuwa na siku nilitaka kuacha, lakini nilijua kukata tamaa kungethibitisha tu dhana zao potovu,” alikiri.

Mabadiliko makubwa yalikuja wakati dereva wa lori alipompuzilia uwezo wake.

“Alisema angesubiri ‘fundi wa kweli’,” alieleza.

Miriam kwa utulivu alimuuliza shida ya lori lake, akatambua kuwa ni sindano ya mafuta (fuel injector) iliyokuwa na hitilafu, na akairekebisha ndani ya saa moja. Dereva huyo aliyeshangazwa si tu alimlipa mara mbili ya bei ya kawaida, bali pia aligeuka kuwa mteja wake wa kudumu.

# EPRA yazindua rasimu ya kanuni kukuza sekta ya nishati ya mimea

NA JOANNE MORAA NA KENEDY OGADA (KNA)

Mamlaka ya Kudhibiti Nishati na Petroli (EPRA) imezindua rasimu ya kanuni mpya zinazolenga kuimarisha sekta ya nishati ya mimea (biofuels) inayokua kwa kasi nchini Kenya. Hatua hii ni sehemu ya juhudi za kufanikisha lengo la taifa la kufikia matumizi ya nishati safi kwa asilimia 100 ifikapo mwaka 2030. Mkurugenzi Mkuu wa EPRA, Daniel Kiptoo, kupitia hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Naibu Mkurugenzi wa Nishati Mbadala, Mhandisi Mungai Kihara, katika mkutano wa ushirikishwaji wa umma uliofanyika Kisumu, alisema kuwa Kanuni za Nishati (Biofuels) za mwaka 2025 zitatoa mwongozo wa kisheria kuhusu uzalishaji, uchanganyaji, usambazaji, na uuzaji wa nishati hiyo kote nchini Kenya. "Kanuni hizi zinalenga kukuza biashara yenye usawa, kuhakikisha ubora na usalama katika mnyororo mzima wa thamani wa nishati ya mimea, kusaidia katika uhifadhi wa mazingira, na kuwezesha ukusanyaji wa takwimu sahihi kwa ajili ya utungaji sera unaotegemea ushahidi," alisema Kiptoo. Alibainisha kuwa rasimu hiyo ya kanuni imekuja wakati ambapo Kenya inazidisha juhudi za kupunguza utoaji wa gesi chafu na kupunguza utegemezi



Mkurugenzi Mkuu wa EPRA Daniel Kiptoo

wa mafuta ya kisukuku. Alitaja mafanikio kama mradi wa ENI katika Kaunti ya Makueni, ambapo kampuni ya mafuta kutoka Italia inatoa mafuta ya mimea kutoka kwa mbegu za mnyonyo kwa ajili ya kusafirishwa hadi kiwanda chao cha kusafishia mafuta nchini Italia. Aliongeza kuwa miradi ya bioethanol inayohusishwa na sekta ya miwa nchini Kenya pia inapata kasi – hasa kwa matumizi ya kupikia kwa njia safi. Mkurugenzi Mkuu alisema kuwa kanuni zinazopendekezwa zitahusu mnyororo mzima wa usambazaji wa biofuels kuanzia uzalishaji na uagizaji hadi kwenye hifadhi, upakiaji, uchanganyaji, na uuzaji. Miongoni mwa masharti muhimu, Kiptoo alieleza kuwa ni pamoja na hitaji la kuchanganya bioethanol na petroli ili kuzalisha "gasohol", na kuongeza kuwa biodiesel inayotokana na mafuta ya mimea na mafuta ya wanyama ni lazima ifuate viwango vilivyowekwa kabla ya kuchanganywa na dizeli ya magari. "Shughuli zote za uchanganyaji lazima zifanyike katika vituo vilivyopewa leseni na EPRA chini ya viwango madhubuti vya ubora, usalama na ulinzi wa mazingira. EPRA itafanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha uzingatiaji kamili," alisema. Kwa upande wake, Mhandisi Kihara alisisitiza umuhimu wa kanuni hizi katika kuleta mageuzi ya sekta ya nishati nchini Kenya. Alisema kuwa kanuni hizo ni muhimu katika kuipanua mchanganyiko wa nishati nchini, kupunguza utoaji wa gesi chafu, na kuongeza upatikanaji wa huduma za kisasa za nishati. "Kanuni hizi si nyaraka tu za kisera; ni mifumo muhimu ya kuwezesha mageuzi na uendelevu katika sekta ya nishati. Tunalenga kufikia asilimia 100 ya nishati safi ifikapo mwaka 2030," alisema. Mhandisi Kihara alisema kuwa kanuni hizo zitahusu matumizi ya nyumbani na viwandani, yakiwemo ya usafiri. Aliongeza kuwa EPRA kwa kushirikiana na Wizara ya Nishati, wanafanya kazi na wakulima hasa katika maeneo ya miwa ya Magharibi mwa Kenya ili kukuza uzalishaji wa ndani wa bioethanol. Naibu Mkurugenzi alisema kuwa mpango huo unatarajiwa kuongeza kipato kwa wakulima na kupunguza utegemezi wa mafuta ya jadi kama kuni na mkaa. "Tunahitaji kila familia iwe na njia safi ya kupikia, na ndiyo maana bioethanol ni muhimu sana," alisema.

# Msukumo mpya wa utengenezaji na uwekaji chapa katika kaunti ili kuchochea biashara nje

NA ESTHER MWANGI NA NELLY KIARIE (KNA)

Serikali za kaunti zimetakiwa kutekeleza mikakati ya kuongeza thamani kwa mazao ya kilimo yanayolengwa kwa mauzo ya nje ili kuvutia bei ya juu kwa mazao ya Kenya katika masoko ya ndani na ya kimataifa. Katibu wa Wizara ya Uendelezaji wa Viwanda, Dkt. Juma Mukhwana, alisisitiza haja ya serikali za kaunti kuendeleza uwekezaji wa viwanda katika maeneo ya ukusanyaji wa mazao, uzalishaji viwandani, chapa, upakiaji, uwekaji wa lebo, na usafirishaji. Alisema juhudi hizo zitasaidia nchi kupunguza utegemezi wa bidhaa za nje. Hatua hiyo pia itachangia maendeleo ya kiuchumi na kusaidia kuanzishwa kwa bidhaa mpya zenye thamani iliyoongezwa zitakazoongeza mapato ya fedha za kigeni. Dkt. Mukhwana alielezea masikitiko yake kwamba Kenya kwa muda mrefu imekuwa ikisafirisha bidhaa ghafi bila kuongeza thamani licha ya uwezo mkubwa wa nchi kushika sehemu kubwa ya masoko ya ndani na kimataifa. Alisisitiza umuhimu wa kuendeleza biashara ya bidhaa zilizoboreshwa. Akitambua kuwa bidhaa nyingi za kimataifa huongezewa mazao ya Kenya, Dkt. Mukhwana alisema serikali inashirikiana na serikali za kaunti pamoja na wadau wa serikali na wale wa mashirika yasiyo ya serikali kuandaa mfumo wa kuanzisha na kuendesha Mbuga za Kaunti za Ukusanyaji na Uendelezaji Viwanda (CAIPs). Alisema mbuga hizo zimeundwa kuendeleza ukuaji kupitia utofauti wa mauzo ya nje ya Kenya, kuongeza thamani, kuunda bidhaa mpya, na kufungua masoko mapya. Dkt. Mukhwana alisema kaunti zinapaswa kuanza maandalizi ya uanzishaji wa mbuga za viwanda kupitia miradi kama ujenzi wa vituo vya ukusanyaji



Katibu katika Idara ya Ustawishaji Viwanda, Wizara ya Uwekezaji, Biashara na Viwanda (MITI), Dkt Juma Mukhwana, akihutubia wanahabari kando ya kikao cha Kamati ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Kiufundi (NTIC) kuhusu Mjumuisho wa Kaunti na Viwanda.

wa mazao ya kilimo vilivyo na miundombinu inayohitajika kwa ajili ya kuhifadhi baada ya mavuno kabla ya kupelekwa kusindikwa, pamoja na kuwaunganisha wakulima katika vikundi au ushirika kwa ajili ya masoko ya pamoja. Alizitaka kaunti kushirikiana na serikali kuu kuunda na kudumisha mazingira yatakayowezesha ukuaji wa viwanda vinavyolenga kuuza nje bidhaa, kwa kutumia faida za uchumi wa viwanda mkubwa, miundombinu ya pamoja, na upatikanaji wa masoko ya kimataifa. Ili kuanzisha CAIPs nchini Kenya, Katibu Mkuu alibainisha kuwa inahitajika mbinu jumuishi inayolenga utambuzi wa bidhaa, uchambuzi wa soko, maendeleo ya miundombinu, na ujenzi wa uwezo. Alisema kaunti zinapaswa kwanza kubaini bidhaa zenye ushindani mkubwa na mahitaji makubwa ya soko katika maeneo yao, na kuhakikisha kuwepo kwa minyororo ya ugavi ya kutosha, akiongeza kuwa miundombinu kama barabara, umeme, maji, mtandao wa intaneti na usafiri ni muhimu kwa ufanisi wa mbuga hizo. "Kaunti lazima ziwape mafunzo wafanyakazi na zitoe msaada kwa Biashara Ndogo, za Kati na za Kati (MSMEs) kwa kuwa ni kiungo muhimu kwa mafanikio ya mbuga hizi," aliongeza Katibu huyo. Dkt. Mukhwana alitoa matamshi hayo wakati wa kikao cha Kamati ya Kitaifa ya Utekelezaji wa Kiufundi (NTIC) kuhusu CAIPs kilichofanyika katika Taasisi ya Mafunzo ya Viwanda Kenya (KITI) mjini Nakuru. Tukio hilo liliwaleta pamoja Maafisa Wakuu wa Kaunti kutoka Nakuru, Busia, Kakamega, Bungoma, Kwale na Kisii katika kujadili mfumo wa sera wa CAIPs. Katibu huyo alisema serikali za kaunti zinaweza kusaidia mbuga za viwanda kwa kutoa msamaha wa kodi, ruzuku, na mchakato wa utoaji wa vibali ulio rahisi, pamoja na kushiriki katika uendelezaji wa mbuga hizo kwa lengo la kuvutia wawekezaji na kuhakikisha upatikanaji wa wafanyakazi wenye ujuzi kupitia programu za mafunzo.

REPUBLIC OF KENYA

## COUNCIL OF LEGAL EDUCATION

### VACANT POSITION

The Council of Legal Education is established under the Legal Education Act, CAP 16B. The core functions of the Council of Legal Education are to regulate Legal Education and training, license and supervise Legal Education providers, conduct the Advocates Training Program (ATP) Examination, recognize and approve qualifications in Law obtained outside Kenya and advise the Government on matters relating to legal education and training.

To effectively deliver on its mandate, the Council wishes to competitively recruit a **full-time** high-caliber officer to the following position.

| No. | Position | Reference | Job Grade | No. of Positions |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Senior Corporate Communication Officer | CLE/ JOB-066/ 2025 | CLE 6 | 1 |

For detailed descriptions of the jobs and application process, visit the careers page on our website, **www.cle.or.ke.**

Applications should reach the undersigned on or before **12th August 2025.**

**AG. SECRETARY/CHIEF EXECUTIVE OFFICER**
**COUNCIL OF LEGAL EDUCATION**
**P. O. BOX 829 - 00502**
**KAREN, NAIROBI**

KENYA VISION 2030

REPUBLIC OF KENYA

## MINISTRY OF ROADS AND TRANSPORT

### STATE DEPARTMENT FOR ROADS

### JOB ADVERTISEMENT

Applications are invited from qualified persons for the following positions shown below:

| VACANCY NO | JOB TITLE | CSG | POSTS |
|---|---|---|---|
| 2/2025 | Housekeeping Assistant I | 13 | 3 |
| 3/2025 | Driver Instructor III KIHBT | 13 | 7 |
| 4/2025 | Plant Operator Instructor III KIHBT | 13 | 8 |
| 5/2025 | Housekeeping Assistant III | 15 | 27 |
| 6/2025 | Cook III | 15 | 23 |
| 7/2025 | Waiter Assistant III | 15 | 5 |
| 8/2025 | Artisan III (General Power Electrician) | 15 | 3 |
| 9/2025 | Artisan Tailoring III | 15 | 3 |
| 10/2025 | Artisan Auto Electrician Mechanic III | 15 | 15 |
| 11/2025 | Artisan Motor Vehicle Mechanic III | 15 | 10 |
| 12/2025 | Artisan Mechanical III | 15 | 6 |
| 13/2025 | Artisan Building III | 15 | 4 |
| 14/2025 | Artisan Plant Mechanic III | 15 | 16 |
| 15/2025 | Artisan Spray Painter III | 15 | 4 |
| 16/2025 | Artisan Panel Beater III | 15 | 5 |
| 17/2025 | Artisan Upholster III | 15 | 4 |
| 18/2025 | Plant Operator III | 15 | 11 |
| 19/2025 | Driver II (Light & Heavy Commercial | 15 | 12 |
| 20/2025 | Security Warden III | 15 | 23 |

Interested and qualified persons are requested to make their applications by completing one PSC2 ***(Revised 2016)*** application form. The form may be downloaded from the Public Service Commission's websites: **www.publicservice.go.ke**

For more details on salary scale, requirements for appointment, duties and responsibilities, visit the following website **www.roads.go.ke.**

Completed PSC 2 (2016) application form can be sent to: -

**The Principal Secretary**
**State Department for Roads**
**Ministry of Roads and Transport**
**P.O. Box 30260-00100 Nairobi**

**OR**

Hand delivered to the **State Department for Roads Human Resource Management registry, Transcom House, 5th Floor** on or before **22nd August, 2025.**

REPUBLIC OF KENYA

## MINISTRY OF INFORMATION, COMMUNICATION AND THE DIGITAL ECONOMY

***MEDIA COUNCIL ACT, 2013***

### DECLARATION OF VACANCIES

**IN ACCORDANCE** with Section 7(2) of the Media Council Act, 2013 ("the Act"), the Cabinet Secretary for Information, Communications and Digital Economy declares vacancies in the positions of Four Members of the Media Council of Kenya.

Qualified candidates are invited to apply for the post. The applications shall be forwarded to the Selection Panel pursuant to Section 7(3) of the Act within Seven (7) days of the publication of this Notice.

**A. QUALIFICATION FOR APPOINTMENT AS MEMBER OF THE COUNCIL**

A person shall be qualified for appointment as a member of the council under Section 8 of the Act, if that person is-

i. A citizen of Kenya
ii. Holds a degree from a university recognised in Kenya
iii. Has knowledge and experience of at least 10 years in matters relating to the following fields-

   a) Law;
   b) Journalism;
   c) Finance;
   d) Gender and Human Rights;
   e) Performing Arts;
   f) Advertising;
   g) Public Relations;
   h) Religious Studies;
   i) Communication;
   j) Humanities and Social Sciences; or
   k) Information Technology.

iv. Meets the requirement of Chapter Six of the Constitution of Kenya, 2010; and
v. Has had a distinguished career in their respective fields.

***Women, persons with disabilities, people from minority and marginalised groups are encouraged to apply.***

**B. DISQUALIFICATION FOR APPOINTMENT AS A MEMBER OF THE COUNCIL**

A person shall not be qualified for appointment as member of the Council under Section 8(2) of the Act, if that person-

i. Is a Member of Parliament or County Assembly;
ii. Is an Official of a governing body of a political party;
iii. Has at any time within the preceding 5 years, held a political office;
iv. Is an undischarged bankrupt;
v. Has been convicted of a felony;
vi. Has benefitted from, or facilitated an unlawful or irregular allocation, acquisition or use of land or other public property; or
vii. Has been removed from office for contravening the provisions of the Constitution or any other written law;

**C. TERMS OF SERVICE**

The members shall hold office for a period of three (3) years and shall be eligible for re-appointment for a further and final term of three (3) years.

**D. HOW TO APPLY**

(a) All applications **(manual and online)** should be accompanied by detailed curriculum vitae, copies of relevant academic and professional certificates, testimonials and other relevant supporting documents. Scanned copies of these documents must accompany online application.
(b) A copy of the National Identity Card or Passport should be appended.
(c) All applications should be clearly marked, ***"Application for position of Member, Media Council of Kenya"*** and submitted in any **ONE** of the following ways:

(i) Manual applications should be hand delivered to the reception desk on **10th Floor of Teleposta Towers, off Koinange Street**
(ii) Online applications should be emailed to **moictjobs@information.go.ke**
(iii) Applications through the post office should be addressed to:

**Selection Panel for the Selection of the Member of the Media Council of Kenya**
**Ministry of Information Communication and the Digital Economy**
**Teleposta Towers**
**P.O Box 30025-00100**
**NAIROBI**

**Note:**
(i) The names of all applicants and the shortlisted candidates will be published under section 7(7) of the Media Council Act in the Kenya Gazette, and in at least two daily newspapers of national circulation and the website of the Ministry of Information, Communication and Technology--**www.information.go.ke.**
(ii) Shortlisted applicants will be required to obtain clearance from the following bodies.
- Kenya Revenue Authority
- Higher Education Loans Board
- Ethics and Anti-Corruption Commission
- Directorate of Criminal Investigation **(certificate of good conduct)**; and
- Credit and Reference Bureau

**All applications should be received before 5.00 pm on Monday, 4th August 2025.**

A copy of this advertisement can also be obtained from the Ministry of Information Communications and Technology website **www.information.go.ke**, The Media Council of Kenya website **www.mediacouncil.or.ke** and from the Government Advertising Agency website **www.mygov.go.ke.**

# SOCIAL HEALTH AUTHORITY (SHA)

## DECLARATION OF VACANCIES

The **Social Health Authority (SHA)** is a State Corporation established under the **Social Health Insurance Act, 2023** and mandated to provide financial risk protection for Kenyan residents by facilitating equitable access to quality healthcare. SHA is responsible for administering the Social Health Insurance Fund, Primary Healthcare Fund, and Emergency, Chronic, and Critical Illness Fund in collaboration with stakeholders.

To enhance institutional capacity and deliver on its mandate, the SHA Board seeks to recruit visionary, result-driven, and experienced professionals for the following Senior Management positions.

| S/NO | DESIGNATION | SHA GRADE | NO OF POSITIONS |
|---|---|---|---|
| 1. | Director, Provider and Beneficiary Management | 2 | 1 |
| 2. | Director, Benefits & Claims Management | 2 | 1 |
| 3. | Director, Corporate Services | 2 | 1 |
| 4. | Director, Funds & Finance Management | 2 | 1 |
| 5. | Director, Internal Audit | 2 | 1 |
| 6. | Deputy Director, County Coordination | 3 | 1 |
| 7. | Deputy Director, Legal Services | 3 | 1 |
| 8. | Deputy Director, Human Resource Management & Development | 3 | 2 |
| 9. | Deputy Director, Administration | 3 | 1 |
| 10. | Deputy Director, Corporate Communication | 3 | 1 |
| 11. | Deputy Director, Information & Communication Technology | 3 | 1 |
| 12. | Deputy Director, Finance & Accounts | 3 | 1 |
| 13. | Deputy Director, Funds Management | 3 | 1 |
| 14. | Deputy Director, Supply Chain Management | 3 | 1 |
| 15. | Deputy Director, Internal Audit | 3 | 2 |
| 16. | Deputy Director, Claims Management | 3 | 1 |
| 17. | Deputy Director, Benefits Management | 3 | 1 |
| 18. | Deputy Director, Registration and Compliance | 3 | 1 |
| 19. | Deputy Director, Provider Management | 3 | 1 |
| 20. | Deputy Director, Planning & Linkages | 3 | 1 |
| 21. | Assistant Director, County Coordination | 4 | 1 |
| 22. | Assistant Director, Legal Services | 4 | 2 |
| 23. | Assistant Director, Human Resource | 4 | 2 |
| 24. | Assistant Director, Administration | 4 | 2 |
| 25. | Assistant Director, Corporate Communication | 4 | 1 |
| 26. | Assistant Director, Customer Experience | 4 | 1 |
| 27. | Assistant Director, ICT | 4 | 1 |
| 28. | Assistant Director, Fund Management | 4 | 2 |
| 29. | Assistant Director, Finance and Accounts | 4 | 2 |
| 30. | Assistant Director, Supply Chain Management | 4 | 1 |
| 31. | Assistant Director, Internal Audit | 4 | 3 |
| 32. | Assistant Director, Claims Management | 4 | 2 |
| 33. | Assistant Director, Benefits Management | 4 | 2 |
| 34. | Assistant Director, Registration and Compliance | 4 | 2 |
| 35. | Assistant Director, Provider Management | 4 | 1 |
| 36. | Assistant Director, Planning & Linkages | 4 | 2 |
| 37. | Principal Officer, Claims Management | 5 | 15 |
| **TOTAL** | | | **64** |

To access full advertisement, including detailed job descriptions, core functions, and person specifications, kindly visit the SHA website at https://recruitment.sha.go.ke/

**APPLICATION REQUIREMENTS**
Applicants must satisfy the requirements of Chapter Six of the Constitution of Kenya by submitting valid and current copies of the following:

1. Certificate of Good Conduct from the Directorate of Criminal Investigations.
2. Tax Compliance Certificate from the Kenya Revenue Authority.
3. Clearance Certificate from the Higher Education Loans Board (HELB).
4. Clearance Certificate from the Ethics and Anti-Corruption Commission (EACC).
5. Report from a Credit Reference Bureau (CRB).

**HOW TO APPLY**
Interested candidates should submit their applications, including:

- A detailed curriculum vitae.
- Copies of academic and professional certificates.
- A cover letter demonstrating suitability for the position.
- Contacts of at least three professional referees.

Applications should be addressed to:
**The Chairperson**
**Social Health Authority**
**P. O Box 30443-00100**
**Ragati Road**
**NAIROBI**

Applications can be submitted online on https://recruitment.sha.go.ke/or physically delivered to SHA building 10th floor by clearly marking the position applied for on the envelope.

**DEADLINE**
All applications must be received by **5.00pm 19th August 2025**.

**TERMS OF SERVICE**
A competitive remuneration package as advised by the Salaries & Remuneration Commission will be offered to the successful candidate.

**SHA is an equal opportunity employer committed to diversity and gender equality. Canvassing will lead to automatic disqualification. Only shortlisted candidates will be contacted.**

MyGov.
Julai 29, 2025
NAIROBI-KENYA I TOLEO No. 5/2025-2026

A PUBLICATION OF
**Government Advertising Agency**
Telposta Towers, Kenyatta Ave/ Koinange Street
P.O Box 30025-00100,
Nairobi Kenya
Telephone: (+254) 4920000 / 1
E-Mail: mygovads@gaa.go.ke

# KEBS yapata kibali cha kimataifa kwa uthibitishaji wa bidhaa na maabara

NA YOBESH ONWONG'A (MYGOV)




**Mkurugenzi Mtendaji wa KENAS Dkt Walter Ongeti na Mkurugenzi Mkuu wa KEBS Esther Ngari washikilia cheti cha kuidhinishwa na ISO/IEC 17065.**

Huduma ya Uidhinishaji ya Kenya (KENAS) imetunuku rasmi Mamlaka ya Viwango ya Kenya (KEBS) ithibati mbalimbali za kimataifa, hatua kubwa inayoboresha ubora wa bidhaa, usalama wa taarifa, na ushindani wa biashara katika ukanda huu.

Katika hafla ya kukabidhi vyeti iliyohudhuriwa na viongozi wa ngazi ya juu, KENAS ilitangaza kuwa KEBS imeidhinishwa kwa viwango vya kimataifa vya ISO/IEC 17065 kama Shirika la Udhibitishaji wa Bidhaa, ISO/IEC 17043 kama Mtoa Huduma wa Majaribio ya Ulinganisho (Proficiency Testing), na upanuzi wa wigo wake wa udhibitishaji wa Mifumo ya Usimamizi (Management Systems Certification Body) ili kujumuisha ISO/IEC 27001:2022 kwa Usimamizi wa Usalama wa Taarifa (ISMS). KEBS pia ilipata ithibati chini ya mpango wa African Certification of Agricultural Products (ACAP), kulingana na kiwango cha ARS/AES 01:2014 — mafanikio makubwa kwa uendelevu wa kilimo na uwekaji alama wa mazingira barani Afrika.

"Huu ni wakati wa kujivunia kwa miundombinu ya ubora ya Kenya," alisema Dkt. Walter Ongeti, Mkurugenzi Mtendaji wa KENAS. "Kwa kuiidhinisha KEBS kwa viwango hivi vinavyotambulika kimataifa, tunaimarisha imani ya watumiaji huku tukifungua fursa kubwa kwa biashara za Kenya katika sekta za kilimo, viwanda, na teknolojia."

Dkt. Ongeti alieleza kuwa ISO/IEC 17065 ni kiwango cha kimataifa kinachothibitisha uwezo wa KEBS kuthibitisha bidhaa—kama alama ya viwango (S-Mark), Alama ya Almasi (Diamond Mark), na Alama ya Uboreshaji wa Chakula (Food Fortification Mark)—kupitia tathmini kali na isiyoegemea upande wowote.

"Kinahakikisha kwa watumiaji wa ndani na masoko ya nje kuwa bidhaa hizo zinakidhi matakwa ya usalama, afya, na utendaji," alisema.

Mkurugenzi huyo alifichua kuwa KEBS imekuwa shirika la pili katika Afrika Mashariki kuidhinishwa na KENAS kwa ISO/IEC 17065, baada ya Shirika la Viwango la Burundi (BBN). Alisema kuwa S-Mark ni ya lazima kwa bidhaa nyingi zinazouzwa Kenya, na hivyo kufanya ithibati hii kuwa kichocheo muhimu cha usalama wa watumiaji na ulinganifu wa kibiashara.

Akizungumzia ISO/IEC 17043 kama Mtoa wa Majaribio ya Ulinganisho, Dkt. Ongeti alisema inahakikisha kuwa KEBS inaweza kutoa vipimo vya kuaminika vya maabara kwa ajili ya kulinganisha usahihi wa matokeo kati ya maabara mbalimbali nchini na katika ukanda.

"Hii inapunguza gharama kwa maabara za Kenya ambazo hapo awali zililazimika kupata huduma hizi kutoka Mashariki ya Kati au maeneo mengine ya Afrika. Kupitia hii, KENAS inaimarisha mfumo wa maabara nchini na kuwezesha maabara za ndani kutimiza masharti ya ithibati, hivyo kuchochea uwekezaji kwenye huduma za maabara," alisema.

Zaidi ya hayo, alieleza kuwa ISO/IEC 27001:2022 – Usimamizi wa Usalama wa Taarifa ni upanuzi wa wigo wa KEBS chini ya ISO/IEC 17021-1, unaoiwezesha kuthibitisha mashirika kuhusu Usimamizi wa Usalama wa Taarifa (ISMS) kwa mujibu wa ISO/IEC 27001:2022.

"Hii inakuja wakati ambapo vitisho vya kimtandao na hatari za faragha ya data vinaongezeka. Mabenki, kampuni za teknolojia, taasisi za serikali, na watoa huduma wa 'cloud' sasa wanaweza kutafuta ithibati ya usalama wa kimtandao inayotambulika kimataifa hapa nchini," alibainisha Dkt. Ongeti.

Mkurugenzi huyo alisema kuwa chini ya Shirika la Kanda la Viwango la Afrika (ARSO), KENAS iliidhinisha KEBS kuthibitisha bidhaa za kilimo chini ya mpango wa ACAP — mpango wa uthibitisho endelevu wa bara zima unaozingatia kiwango cha ARS/AES 01:2014.

# Nchi za EAC zahimizwa kuoanisha uzalishaji wa chai ya orthodox

NA SADIK HASSAN, KNA



**Washikadau wa sekta ya chai asili wakati wa maonyesho ya kwanza ya chai ya Kiafrika katika Hoteli ya Sapphire Mombasa. Picha: Andrew Hinga**

Nchi za Afrika Mashariki zinapaswa kuoanisha viwango vyao vya uzalishaji wa chai ili kunufaika kikamilifu na ongezeko la mahitaji ya chai ya orthodox duniani.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Africa Orthodox Tea ulioandaliwa na Chama cha Wauzaji Chai Afrika Mashariki (East African Tea Trade Association) jijini Mombasa, Mkurugenzi Mkuu wa Bodi ya Chai ya Kenya (TBK), Willy Mutai, alisema Afrika imekuwa kinara kwa muda mrefu katika uzalishaji wa chai aina ya black CTC (crush, tear, curl), ikichangia asilimia 12 ya chai katika soko la kimataifa.

Hata hivyo, alibainisha kuwa bei ya chai ya CTC imekuwa ikidorora au kudumaa katika miaka ya hivi karibuni, jambo ambalo limeathiri pakubwa mapato ya wakulima.

"Afrika sasa imefika katika kipindi cha mabadiliko ya kimkakati. Watumiaji wa kimataifa wanatafuta bidhaa zenye asili halisi, simulizi za kipekee, manufaa ya kiafya na uwazi wa uzalishaji. Chai ya orthodox inakidhi mahitaji hayo kikamilifu — hutengenezwa kwa mikono, ina ladha mbalimbali, inatokana na urithi wa kitamaduni, na imelenga soko la kifahari duniani," alisema Mutai.

Aliongeza kuwa chai nyeusi ya orthodox ina thamani ya juu na uwezo mkubwa wa kibiashara, hivyo inatoa fursa ya kuibadilisha chai ya Afrika kutoka bidhaa ya kawaida ya wingi kuwa bidhaa ya kifahari yenye chapa.

## KWA UFUPI

### Uingereza, Uturuki zajenga madarasa ya ECDE Wajir

NA HAMDI BUTHUL

Serikali ya Kaunti ya Wajir inashirikiana na Serikali za Uingereza na Uturuki kuboresha elimu ya msingi katika kaunti hiyo.

Kaunti hiyo imezindua madarasa mapya ya Elimu ya Awali (ECDE) na kusambaza vifaa vya kujifunzia katika Shule za Msingi za Hodhan na Barwako.

Msaada huo, unaotekelezwa kupitia Ofisi ya Mambo ya Nje, Jumuiya ya Madola na Maendeleo ya Uingereza (FCDO) pamoja na Shirika la Ushirikiano na Uratibu la Uturuki (TIKA), unalenga kuboresha upatikanaji wa elimu ya awali kwa watoto kote kaunti ya Wajir.

Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Kamishna wa Kaunti ya Wajir Karuku Ngumo alisema kuwa msaada katika hatua ya awali ya elimu utazaa matunda ya muda mrefu.

"Msingi wa elimu huanza katika kiwango cha ECDE. Tukiwapa wanafunzi mazingira rafiki ya kujifunzia, tunapunguza ndoa za mapema, kuacha shule na mimba za mapema," alisema Ngumo.

Ngumo aliongeza kuwa mpango huo utaongeza idadi ya wanaojiandikisha shuleni na kuhamasisha watoto kuhusu umuhimu wa elimu.

Naibu Mkurugenzi wa Maendeleo wa FCDO, Bi. Eduarda Mendonça Gray, alisema Uingereza imejitolea kusaidia elimu katika Kaunti ya Wajir kupitia mafunzo ya walimu na utoaji wa vifaa vya kujifunzia.

"Tuko hapa kuwasaidia watoto wapate elimu bora ili siku moja wawe magavana au hata marais. Ushirikiano huu ni wa kipekee duniani, ambapo Uingereza inatoa mafunzo kwa walimu na TIKA inasaidia miundombinu," alisema Gray.

Aliongeza kuwa ushirikiano huo, chini ya Mpango wa Inspire, umewafunza walimu zaidi ya 500 na kusaidia shule 264 katika Wajir kwa vifaa vya kujifunzia.

Gavana wa Wajir Ahmed Abdullahi alisema kuwa vituo 368 vya ECDE katika Kaunti ya Wajir kwa sasa vinahudumia wanafunzi 28,686, wakihudumiwa na walimu 543 waliohitimu.

### Mamlaka yazima uuzaji nje wa macadamia ghafi



NAWANGARI NDIRANGU, KNA

Mamlaka ya Kilimo na Chakula (AFA) imetoa notisi inayopiga marufuku usafirishaji wa karanga za macadamia ambazo bado hazijachakatwa au kusafishwa.

Mkurugenzi Mkuu wa AFA, Dkt. Bruno Linyiru, alisema katika taarifa kwamba shehena kadhaa za karanga ghafi za macadamia, zilizodaiwa kuwa katika usafiri kupitia Kenya, zilinaswa katika maeneo mbalimbali ya mipaka.

Alibainisha kuwa ukamataji huo umefanywa kwa mujibu wa utekelezaji wa Sheria ya Mazao ya Kilimo ya mwaka 2013, pamoja na Kanuni za Mazao ya Karanga na Mafuta ya mwaka 2020, zinazolenga kulinda sekta ya uchakataji wa karanga humu nchini.

"Mamlaka inasisitiza kwamba hakuna karanga ghafi za macadamia zitakazoruhusiwa kusafirishwa nje kupitia au kutoka Kenya, bila kujali zinakotoka, na kwamba wauzaji kutoka mataifa ya kigeni wanaokusudia kufanya biashara ya karanga ghafi wanashauriwa kutumia bandari mbadala za nje na kuepuka kupitisha bidhaa hizo kupitia Kenya," alionya.

Dkt. Linyiru aliongeza kuwa hatua hii inalenga kuwaunga mkono wakulima na wachakataji wa ndani kwa kuendeleza uchakataji wa ndani na ukuzaji wa viwanda vya hapa nchini.

"Mwananchi yeyote au mdau anayetaka ufafanuzi wowote anaweza kuwasiliana na Mamlaka kupitia barua pepe info@afa.go.ke," alisema.

REPUBLIC OF KENYA
GAA GOVERNMENT ADVERTISING AGENCY
KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD
DESIGN AND EDITING OF MYGOV WEEKLY BY THE KENYA YEARBOOK EDITORIAL BOARD
SHA Building , 4th Floor, P.O. Box 34035-00100
Tel: 0202715390 / 0757029456
Email: mygovads@gaa.go.ke
www.gaa.go.ke